KIMA WEKUNDU

Ngazi ya Pili

Ali Mwalim Rashid

21st Century Basic Education Program(TZ21)
P O Box 34618
Dar es salaam

© Ali Mwalim Rashid,2014

Mchoraji: Abdul Gugu
Usanifu: Sisi Illustrators

ISBN 978 9987 9448 5 9

Kitabu hiki kimechapishwa na TZ21 kwa msaada wa watu wa marekani kupitia Shirika la Misaada la Marekani (USAID) na kuwezeshwa na Creative Associates International.Yaliyomo katika kitabu hiki yanatokana na mwandishi na mchapishaji wake na hayawakilishi maoni na msimamo wa USAID wala serikali ya Marekani.

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kutafsiri,Kupiga chapa au kukitoa kitabu hiki sehemu yake kwa njia yoyote ile bila idhini ya 21st Century Basic Education Program(TZ21).

Kima wekundu ni wanyama waliopo Zanzibar.
Wapo kwa wingi katika kisiwa cha Unguja.

Miili ya Kima hawa ina manyoya ya rangi nyekundu.
Rangi hiyo inavutia, inawafanya wapendeza sana.

Kima wekundu wanapenda sana kuishi msituni. Unguja wanaishi kwa wingi katika msitu wa Jozani.



Wanyama hawa hukaa kwenye miti.
Hurukia matawi ya miti hii na ile.

Wakati mwengine Kima wekundu hutembea ardhini.
Hutembea kwa ajili ya kutafuta chakula.

Kima hawa wanapenda kula matunda machanga na majani ya miti.
Wanakula maua na vilele vya miti.



Watalii wengi hufika msitu wa Jozani kila mara. Wanafunzi wengi hupendelea kuwaona kima wekundu.

Wazungu wengi kutoka Ulaya nao pia hutembelea msitu huo.

Wanapofika huko huwatazama Kima wekundu kwa furaha.



Wazungu hao hucheza sana na Kima hawa adimu.
Wanawapa mikono na kuwapiga picha.

Hakika kima hawa ni marafiki wa binadamu.
Ni lazima kuwalinda kwa hali na mali.

Maswali.

Jibu maswali haya:

1. Kima wekundu wanapatikana kwa wingi wapi?
2. Msitu wa Jozani wanaishi wanyama gani?
3. Watalii hufika msitu wa Jozani kufanya nini?
4. Kima wekundu wana miguu mingapi.
5. Chora picha ya kima wekundu katika buku lako wakiwa katika matawi ya miti?

Msamiati

Kisiwa : Sehemu ya ardhi iliyozungukwa na bahari au ziwa.

Manyoya : Aina ya nywele zinazoota mwilini mwa mnyama

Watalii : Watu wanaotembelea sehemu zenye kuvutia.

Wazungu : Watu wenye asili ya Ulaya.

Adimu : Kutokupatikana sana

Ulaya : Bara ambalo linaishi Wazungu

Msitu : Sehemu yenye miti mingi.

Chemsha Bongo

Andika maneno yafuatayo katika jedwali ulilopewa.

K		W						A					
A													
		M					I						
W												Z	
			W			K							
	Z												
I						M					Y		
	I		U									R	

A. Kwenda kulia.
1. Manyoya
2. Kima wekundu
3. Majani
4. Kuwalinda

B. Kwenda chini:
1. Jozani
2. Watalii
3. Wanyama
4. Zanzibar